

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz



SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA SABA WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI UTAKAOANZA TAREHE 27 SEPTEMBER, 2017

Mkutano wa Saba wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 27 Septemba, 2017, saa 3:00 asubuhi.

SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA.

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Maswali na Majibu.

Maswali 136 yameratibiwa kwa ajili ya kujibiwa kwenye Mkutano huu.

2. Miswada ya Sheria

Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na kusomwa kwa mara ya Kwanza katika Mkutano wa Mei - June, 2017 itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa katika Mkutano huu wa Saba.

Miswada yenyewe ni:-

- i) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- ii) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

3. Ripoti za Wizara za SMZ Kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza.

4. Taarifa ya Serikali Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

5. Miswada mbali mbali itakayosomwa kwa mara ya Kwanza.

6. Mengineyo kwa Ruhusa ya Spika.

Raya Issa Msellem
Katibu
Baraza la Wawakilishi
Zanzibar

Tarehe 25 Septemba, 2017